WiLDAF

Shirika la Wanawake Katika Sheria na Maendeleo Barani Afrika
(WiLDAF)

# UKATILI MAJUMBANI TANZANIA
# HAJA YA MABADILIKO YA KISHERIA

## HAJA YA KUUNDWA KWA SHERIA
## DHIDI YA UKATILI MAJUMBANI

## MUHTASARI WA SERA

Suala la: 1

Julai, 2021

**Shirika la Wanawake Katika Sheria na Maendeleo Barani Afrika (WiLDAF)**

# UKATILI MAJUMBANI TANZANIA

## HAJA YA KUUNDWA KWA SHERIA DHIDI YA UKATILI MAJUMBANI

## MUHTASARI WA SERA

**Suala la: 1**

**Julai, 2021**

## UTANGULIZI

Ukatili majumbani ni pamoja na vitisho vya kimapenzi, shambulio la kimwili, ukatili wa kijinsia, na /au tabia nyingine za ukatili kama sehemu ya matumizi ya nguvu na udhibiti unaofanywa na mwenza mmoja dhidi ya mwingine. Ukatili majumbani pia unajumuisha ukatili wa kimwili, ukatili wa kingono, vitisho, ukatili wa kiuchumi, ukatili wa kihisia / kisaikolojia na huenda zaidi mpaka kwa watu zaidi ya wanandoa wanaoishi katika nyumba moja. Ukatili majumbani unaweza kutokea kwa mtu yeyote wa rangi yoyote, umri, dini, au jinsi yoyote. Kwa kuongeza, inaweza kutokea ndani ya mahusiano mbalimbali, ikiwa ni pamoja na wanandoa, kuishi pamoja, au mahusiano ya kawaida ya kimapenzi.

Muhtasari huu umetokana na takwimu zilizopatikana na mapitio ya sera, mifumo ya kisheria, na takwimu nyingine zilizofanyiwa utafiti kuhusu Ukatili majumbani nchini Tanzania. Kwa kuchambua mwenendo wa sheria za kitaifa, mikakati, mipango, uratibu, na vikwazo vya kushughulikia ukatili majumbani. Muhtasari huu unalenga kushawishi kutungwa kwa sheria kamili dhidi ya ukatili majumbani nchini Tanzania. Zaidi ya hayo, muhtasari huu unashauri kutengenezwa kwa mifumo mizuri ya kisheria na njia mbalimbali za kuzuia na kukabiliana na ukatili majumbani.

Muhtasari huu unatoa mapendekezo kwa wabunge na watunga sera kwa kuchukua hatua za kutunga Sheria ya Ukatili majumbani nchini Tanzania.

# UKUBWA WA TATIZO LA UKATILI MAJUMBANI TANZANIA

## a) Ukatili Dhidi ya Wenza

Ukatili dhidi ya wenza ni moja kati ya aina za ukatili majumbani nchini Tanzania. Utafiti wa Idadi ya Watu na Afya (TDHS), 2015-2016 umebaini kuwa;

Asilimia 40 ya wanawake walioolewa wamewahi kufanyiwa vitendo vya ukatili wa kimwili, kijinsia, au kihisia kutoka kwa wenzi wao.

- Asilimia 39 ya wanawake wamewahi kufanyiwa ukatili wa kimwili; Kama kupigwa na kuchomwa na vitu vyenye ncha kali.
- Asilimia 4 ya wanawake wamekatwa au kuchomwa kwa kusudi na wenzi wao na wametishiwa au kushambuliwa kwa kisu, bunduki, au silaha nyingine.
- Asilimia 14 ya wanawake walioolewa wamepitia kitendo kimoja au zaidi vya ukatili wa kijinsia, ikiwa ni kulazimishwa kufanya ngono na mwenzi wao.
- Asilimia 36 ya wanawake wamewahi kufanyiwa ukatili wakisaikolojia kwa mfano kutukanwa na wenzi wao.

## b) Ukatili Dhidi ya Watoto

- ✓ Ripoti ya Jeshi la Polisi Tanzania ya mwaka 2020 inaonesha ongezeko la ukatili dhidi ya watoto kwa 26%mwaka 2020, visa 7388 viliripotiwa kote nchini, tofauti na mwaka 2015, ambapo matukio 5,803 yaliripotiwa.
- ✓ Dawati la Jinsia na Watoto la Polisi liliripoti kuwa katika kila miezi mitatu, watoto 21 wanabakwa. Wengi wa wahalifu ni ndugu wa karibu na watu ambao watoto wanawajua na kuwaamini. Nyumbani kumekuwa mahali hatari kwa wanawake na watoto.

## c) Usafirishaji Haramu wa Wanawake na Watoto

- ✓ Nchini Tanzania, usafirishaji haramu wa binadamu unafanyika ndani na nje ya mipaka ya nchi. Kesi nyingi zinahusisha watoto walioajiriwa chini ya ahadi za uongo za elimu nzuri na kutumiwa kama watumishi wa ndani katika sekta ya ngono au sekta ya uvuvi na madini.

## d) Madhara ya Kimwili ya Ukatili Majumbani

Ukatili majumbani husababisha madhara ya kimwili na kisaikolojia kwa waathirika na kuweka afya zao katika hali mbaya na kupelekea maisha yao kuwa hatarini. Ukatili majumbani una athari za kisaikolojia za muda mrefu kama vile msongo wa mawazo na kushindwa kujithamini, hali ambayo inaathiri zaidi uwezo wa mwathirika kustawi.

**Ripoti ya TDHS ilieleza kwamba;**

- ✓ Asilimia 70 ya wanawake ambao wamewahi kupata ukatili wa kimwili au kijinsia wamepata aina moja au zaidi ya majeraha, kama vile kuchanika, michubuko, au maumivu. Halikadhalika, asilimia 15 ya wanawake wamepata majeraha makubwa, mifupa iliyovunjika, meno yaliyovunjika, au majeraha mengine makali kutokana na ukatili kutoka kwa wenza.
- ✓ Aidha, kwa mujibu wa utafiti wa Shirika la Afya Duniani (WHO) kuhusu afya ya wanawake na ukatili dhidi ya Wanawake, asilimia 15 ya wanawake waliojeruhiwa jijini Dar es Salaam na asilimia 23 ya wanawake jijini Mbeya walipoteza fahamu angalau mara moja kutokana na kupigwa.

## e) Kutafuta Msaada

**Ripoti ya TDHS ya mwaka 2016 inaonesha kuwa ;**

- ✓ Asilimia 54% ya wanawake waliofanyia ukatili wa kimwili au wa kijinsia kutoka kwa mtu yeyote waliweza kutafuta msaada kutoka kwa mtu, ikiwa ni ongezeko la asilimia 20 kutoka mwaka 2010. Hata hivyo, theluthi moja ya wanawake (34%) hawajawahi kutafuta msaada au kumwambia mtu yeyote juu wa vitendo vya ukatili walivyofanyiwa.
- ✓ Huko nyuma utafiti wa Shirika la Afya Duniani (WHO) wa mwaka 2004 ulionesha kuwa, asilimia 29 ya wanawake waliopata ukatili wa kimwili jijini Dar es Salaam na asilimia 30 jijini Mbeya hawakuwahi kumwambia mtu yeyote kuhusu ukatili huo. Asilimia 56 ya wanawake ambao hawakutafuta msaada jijini Dar es Salaam, na asilimia 48 jijini Mbeya kwa sababu walidhani ukatili huo ni ‘wa kawaida’ au sio mkubwa wa kutosha kuhitaji msaada.

## SABABU ZINAZOCHANGIA KUKITHIRI KWA UKATILI MAJUMBANI

### a) Mfumo wa kisheria katika kushughulikia Ukatili majumbani

Serikali imefanya juhudi kubwa za kuzuia na kushughulikia ukatili wa kijinsia kwa kutunga sera na sheria. Hata hivyo kuwa na mifumo mingi tofauti ya kisheria, kuwa na sheria mbalimbali zinazoshughulikia kitu kimoja katika mwelekeo tofauti zinaleta mkanganyiko hasa katika tafsiri ya sheria hizo. Sheria hizi ni pamoja na Sheria ya Ndoa, Sura ya 29, Kanuni za Makosa ya Adhabu, Sura ya 16, Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009, Sheria ya Kupambana na Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu Na. 6 ya mwaka 2008, Sheria ya Kimila na Mirathi ya mwaka 1963. Sheria hizi zinatoa mwanya kwa wahalifu wa ukatili kuendelea kutenda ukatili kama ilivyoelezwa hapo chini.

#### i. Sheria ya Ndoa, Sura ya 29 ya Mwaka 1971

Kifungu cha 66 cha Sheria ya Ndoa, kinakatazaadhabu ya viboko kwa mwenza. Hata hivyo, kifungu hiki hakitoi adhabu kwa mwenza atakayefanya kitendo hicho. Isipokuwa, pale tu adhabu hiyo itakapoleta majeraha ya kimwili ambapo atashtakiwa kama kosa la jinai. Vile vile sheria ya ndoa inaruhusu msichana kuolewa akiwa na umri wa miaka 15 kwa idhini ya wazazi au miaka 14 kwa idhini ya mahakama, hii ni aina nyingine ya ukatili majumbani. Zaidi ya hayo, sheria ya ndoa haifafanui ukatili majumbani wala kutafsiri upeo wa ukatili majumbani ili kulinda watoto dhidi ya ndugu wanaoishi katika nyumba moja ya familia.

#### ii. Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16

Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 ni moja ya sheria kongwe nchini Tanzania ilifanyiwa marekebisho yanayojulikana kama Sheria Maalumu ya Makosa ya Kujamiiana (SOSPA) ya mwaka 1998. Hata hivyo, mageuzi yaliyofanywa na SOSPA yaliainisha makosa ya kujamiiana kama vile mashambulizi ya kingono, ukatili wa kingono, na shambulio la aibu linalosababisha madhara halisi ya mwili makosa haya yaliingizwa katika Kanuni ya Adhabu sura ya 16. Hivyo, kama kupigwa au kufanyiwa ukatili wa kingono kwa mke au mtoto hakujasababisha madhara makubwa ya mwili, shtaka la kumshambulia mke kwa kawaida haliwezisimama. Sheria ya Ndoa, ubakaji wa kwenye ndoa pia sio kosa chini ya Kanuni ya Adhabu, wala sheria hii haifafanui ukatili majumbani au kutafsiri wigo wake.

### iii. Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009

Sheria ya Mtoto imetambua kanuni za maslahi bora ya mtoto kama ilivyofafanuliwa katika Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto wa mwaka 1989 na Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto wa mwaka 1990. Sheria ya Mtoto imezingatia masuala yote yanayohusiana na haki za watoto chini ya umri wa miaka kumi na nane. Hata hivyo, sheria hii haifafanui wala kutafsiri ndoa za utotoni kama moja ya aina ya ukatili majumbani dhidi ya watoto. Aidha, Sheria ya Mtoto haitoi mwongozo na adhabu kwa wazazi wanaofanya vitendo vya ukatili majumbani kwa watoto wao ikiwa ni pamoja na kuwalazimisha kuolewa, kuzuia usafirishaji wa watoto wao. vitendo hivyo ni kama vipigo, ukeketaji na matukio mengine ya Ukatili wa watoto. Pamoja na hayo, sheria ya mtoto inaruhusu adhabu ya viboko ambayo ni ukatili dhidi ya watoto.

### iv. Sheria ya Kimila ya Mirathi ya mwaka 1963.

Sheria ya Kimila ya Mirathi (Tangazo la Serikali namba 4) ya 1963 inatumika kwa watanzania wote wazawa wanaofuata mila na desturi zao na wanaorithi kupitia upande wa baba. Sheria ya kimila ni ya kibaguzi na huleta changamoto wanawake, wajane, wanaume, na watoto. Kwa kwa wanawake sheria hii inakataza kumiliki mali zisizohamishika pamoja na ardhi ya ukoo. Vilevile mjane haruhusiwi kurithi mali za marehemu mume wake isipokuwa atarithi kupitia watoto wake. Mjane ambae hajabahatika kuzaa, hupata asilimia 20 ya asilimia 50 ya mali za marehemu mume wake. Watoto wa kike wako katika daraja la mwisho la urithi baada ya mtoto wa kwanza wa kiume na watoto wakiume waliobaki. Pia sheria hii imebagua watoto wakiume kwa kuwagawa kimadaraja kwenye urithi. Hii ni aina mojawapo ya ukatili majumbani na hakuna sheria yoyote nchini Tanzania inayofafanua kunyimwa haki za mirathi kama aina ya ukatili majumbani.

### v. Sheria ya Kupambana na Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu Na. 6 ya mwaka 2008

Sheria hii inaharamisha aina zote za biashara ya kusafirisha watu nchini Tanzania. Hata hivyo, Sheria haitoi upatikanaji mzuri wa huduma au tiba kwa waathirika wa biashara haramu. Biashara ya binadamu wakati mwingine hufanywa na watu wanaoishi ndani ya kaya moja. Aidha, hakuna sheria inayoeleza kwamba usafirishaji haramu kwa wa wanawake na watoto kama aina moja ya ukatili majumbani.

### vi. Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) 2016/17-2021/22

Nia ya serikali ya kupunguza ukatili imeelezwa katika Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA). Chini ya eneo la 1 la utekelezaji wa mpango huu, serikali inakusudia kuimarisha uchumi wa kaya hasa kwa wanawake ili kupunguza ukatili wa kijinsia. Hata hivyo, hatuna sheria inayofafanua kama ukatili za kiuchumi ni ukatili wa kijinsia. Matokeo yake, wanawake wengi wananyimwa haki zao za kiuchumi katika kaya hizi.

Eneo la 2 la utekelezaji, mpango huo unalenga kubadilisha tamaduni hasi pamoja na kukuza tamaduni chanya na kanuni nzuri za kijamii. Baadhi ya viashiria vilivyoangaziwa katika eneo hili ni pamoja na kupunguza matukio ya ukeketaji, ukatili wa kijinsia, mimba za utotoni, ndoa za mapema na ukatili wa kimwili. Hata hivyo, utekelezaji wa mpango huu utaweza kuzaa matunda iwapo kutakua na sheria maalumu inayoshughulikia ukatili majumbani.

### a) Sababu Nyinginezo zinazochochea Ukatili Majumbani

Mbali na changamoto za kisheria, mambo mengine yanayoendeleza ukatili majumbani ni pamoja na;

#### i. Mfumo Dume

Takwimu zinaonyesha asilimia 58 ya wanawake na asilimia 40 ya wanaume wanaafiki kwamba mume ana haki ya kumpiga mke wake angalau kwa moja ya sababu zifuatazo: ikiwa ataunguza chakula, anajibizana naye, kutoka bila kumwambia, anaposhindwa kulea watoto, au anapokataa kufanya naye ngono. Kuendelea kwa mfumo dume kunaweza kuchangiwa na ukosekanaji wa sheria kali dhidi ya wahalifu wa vitendo vya ukatili majumbani.

#### ii. Dini na Imani za Kimila

Baadhi ya viongozi wa dini, wanatumia dini kama chombo cha kukandamiza wanawake. Viongozi hawa huchangia katika kuhalalisha Ukatili dhidi ya wanawake kwa kutumia maandiko ya kidini nje ya muktadha wa dini. Kwa mfano matumizi ya mistari kama mwanaume ni kichwa cha familia, mara nyingi huleta athari kwa jamii kwa kuwachukulia wanawake na wasichana kama vyombo au mali zingine za familia.

### iii. Elimu Duni kwa Wanawake Juu ya Haki zao

Katika maeneo mengi ya Tanzania, wanawake hawajui sheria na haki zao. Hii inasababisha wao kujitenga na mfumo wa kisheria, wakidhani kuwa hakuna chaguo jingine zaidi ya kuteseka katika nyumba zao pale wanapopitia ukatili. Aidha, viwango vya chini vya elimu kwa wanawake husababisha wao kuwa tegemezi kiuchumi kwa wanaume.

### Vikwazo vya Taasisi na Mifumo

Wale wanaotafuta haki hawawezi kupata msaada wa kutosha kutoka kwa Taasisi za Serikali, ukosefu wa sheria wazi ambazo zinafafanua ukatili majumbani na kuweka taratibu za kushughulikia kesi kama hizo. Mbali na hilo, ukosefu wa huduma duni za afya na msaada wa makazi kwa waathirika, na taratibu za gharama kubwa na za muda mrefu za mahakama ni baadhi ya vikwazo vingine ambavyo wanawake wanakabiliwa navyo. Sababu hizi huwavunja moyo wanawake kutafuta msaada kuchochea zaidi hatari zaidi ya ukatili majumbani.

## HAJA YA KUWA NA SHERIA YA UKATILI MAJUMBANI TANZANIA

### i. Ukosefu wa sheria maalum zinazoharamisha ukatili majumbani

Kama ilivyoelezwa mapema, hakuna sheria maalumu nchini Tanzania ambazo zinaharamisha ukatili majumbani. Matokeo yake, kuna ongezeko kubwa la matukio ya ukatili majumbani.

### ii. Uwepo wa Sheria zinazokinzana katika kushughulikia ukatili majumbani

Sheria za Tanzania zinazoshughulikia maswala ya ukatili ni nyingi. Hii inapelekea kukinzana kwa sheria zinazoshughulikia Ukatili majumbani. Kama ilivyoelezwa Sheria ya Ndoa ambayo inakataza mwenza kumpa adhabu mwenza wake bado haijasaidia kukomesha vitendo hivyo kwa sababu ya kushindwa kutoa adhabu kwa mhalifu. Inaachia jukumu hilo la kutoa adhabu kwa Kanuni ya Adhabu, ambayo pia haijaeleza ukatili majumbani. Kuna haja ya kuwa na sheria moja maalum ambayo itashughulikia masuala yote yanayohusiana na ukatili majumbani. Licha ya kuwa na madawati ya jinsia ya polisi yanashindwa kufanya kazi kiufasaha kwa kutokua na sheria moja inayotoa muongozo wa ushughulikiaji wa ukatili majumbani.

Kwa bahati mbaya, hakuna sheria au sera inayofafanua Ukatili majumbani nchini Tanzania. Kama ilivyoelezwa mwanzo kifungu cha 66 cha Sheria ya Ndoa, kinajaribu kutafsiri ukatili lakini haijahusisha vitendo vya ukatili majumbani. Tafsiri kutoka kwa sheria zote mbili haziendi zaidi kujumuisha washirika ambao hawajaoana lakini wako katika mahusiano ya karibu. Mbali na hilo, pia hakijajumuisha ukatili dhidi ya watoto, wanawake wanaonyanyaswa na ndugu ambao hawahusiani kwa damu wanaoishi katika nyumba moja na wasichana wa kazi za nyumbani. Hii haijumuishi sehemu kubwa ya wahusika wa ukatili majumbani, na inazuia wigo wa kushughulikia ukatili majumbani.

### Kukosekana kwa Mahakama Maalumu ya Masuala ya Kifamilia

Masuala ambayo yanahusu ukatili majumbani yanaonekana na watu wengi kama suala la kibinafsi kushughulikiwa na familia na sio hadharani. Tanzania haina mfumo tofauti wa mahakama kwa masuala ya kifamilia, na hivyo kesi za ukatili zinashtakiwa katika mahakama kuu ambako kesi za uhalifu zinafanyika. Kifungu cha 76 cha Sheria ya Ndoa kinatoa mamlaka ya awali katika kesi za ndoa katika Mahakama Kuu, mahakama ya hakimu mkazi, mahakama ya wilaya, na mahakama ya mwanzo. Hata hivyo, mambo yanayoshughulikiwa zaidi katika mahakama hizi ni talaka, kutengana pamoja na matunzo ya watoto.

Ikiwa kupigwa kwa mke au mtoto kunasababisha madhara makubwa ya mwili, shtaka la kumshambulia mke litasimama, na mahakama za jinai zitatumika kushughulikia kesi za ukatili majumbani. Ni changamoto kwa wanawake wengi na wasichana kutoa taarifa kuhusu matukio ya ukatili majumbani kwa sababu ya mifumo ya mahakama. Kwa hiyo, kuna haja ya kutunga Sheria ya Ukatili majumbani ili kuanzisha Mahakama za Familia ambazo zitashughulikia masuala yote yanayohusiana na kesi za ukatili majumbani.

### iii. Huduma duni za msaada kwa waathirika wa Ukatili Majumbani

Wakati mwingine Dawati la Jinsia na Watoto la Polisi linahitajika kuwaweka waathirika wa ukatili majumbani mahabusu kama wahalifu ili kuwaokoa wasirudi nyumbani ambako ukatili umefanywa. Sheria dhidi ya ukatili majumbani inapaswa kutungwa ili kuweka taratibu nzuri za kushughulika na wahalifu wa ukatili majumbani ikiwa ni pamoja na kuwaondoa nyumbani mpaka mashauri yao yatakapokamilika.

### iv. Watuhumiwa wa ukatili ni ndugu wa karibu na watu ambao waathirika wanaamini.

Ripoti ya polisi inaonyesha kwamba wahusika wakuu wa ukatili majumbani ni ndugu wa karibu, ikiwa ni pamoja na wajomba, ndugu wengine, wakwe na hata wazazi. Hii inafanya nyumba kuwa moja ya maeneo hatari zaidi kwa wanawake na watoto. Takribani wanawake 1,583 huuawa na washirika wa karibu na wanafamilia barani Afrika kila mwezi. Kwa hiyo, watu wengi hawasemi au kutoa taarifa kwa kuwa yanafanywa na jamaa au ndugu wa karibu wa familia na jambo hilo ni suala la familia na litatatuliwa ndani ya familia. Hivyo ni vyema kuwa na mifumo ya kisheria madhubuti inayochukua hatua kwa wahalifu wote na wale wanaoficha wahalifu wa ukatili majumbani.

## Mifano bora ya nchi za Afrika zenye sheria dhidi ya ukatili Majumbani

**Afrika Kusini:** Sheria ya Ukatili majumbani Na. 116 ya Novemba 1996 iliandaliwa kwa ushiriki wa wanachama wa Asasi za Kiraia nchini Afrika Kusini. Madhumuni ya Sheria hiyo ilikuwa ni kuwawezesha waathirika wa ukatili majumbani kupata ulinzi wa hali ya juu dhidi ya ukatili majumbani ambao sheria inaweza kutoa na kuanzisha hatua zinazolenga kuhakikisha kuwa vyombo husika vya Serikali vinatoa haki kwa waathirika wa ukatili. Kwa mujibu wa Ripoti za Afrika Kusini, sheria inayoharamisha ukatili majumbani imepunguza matukio ya vurugu kwa hofu ya wahusika kushtakiwa kwa makosa ya jinai na kuongeza idadi ya kesi za ukatili majumbani zilizosajiliwa katika mahakama ya sheria kwa asilimia 40.

**Kenya:** Sheria ya Ulinzi dhidi ya Ukatili majumbani ya mwaka 2015. Kwa miaka mingi nchini Kenya, Ukatili majumbani umefanywa kwa wanaume, wanawake na watoto, na hakukuwa na sheria maalum juu ya uhalifu kama huo. Hata hivyo, mnamo Mei 2015, Sheria dhidi ya ukatili majumbani ilitungwa, kwa lengo la kutoa misaada na ulinzi kwa waathirika wa ukatili majumbani na kuanzisha makosa yasiyo ya kawaida, ambayo ni pamoja na: Ukatili wa kiuchumi, ukatili wa kihisia, ukeketaji, kubughudhiwa na mashemeji, upimaji wa ubikira na ukatili wa kingono katika ndoa. Matokeo yake, kwa mujibu wa ripoti za Kenya, kuna ongezeko la asilimia 25 ya kesi za ukatili majumbani kuripotiwa na ongezeko la asilimia 21 la wanawake wanaopata haki kupitia sheria hii.

**Malawi:** Mwaka 2006, Sheria ya Kuzuia Ukatili majumbani ilipitishwa nchini Malawi. Sheria hiyo ilionyesha dhamira ya Serikali ya kutokomeza ukatili wa kijinsia unaotokea ndani ya uhusiano wa ndani na kutoa msaada bora wa kisheria na huduma nyingine za kijamii kwa watu walioathirika na ukatili majumbani. Hata hivyo, hakuna takwimu maalum juu ya jinsi sheria hii ilivyo saidia kupunguza matukio ya ukatili majumbani lakini sheria imeonesha juhudi na dhamira ya Serikali kushughulikia ukatili majumbani.

### Mapendekezo.

- ✓ Serikali inapaswa kuandaa Sheria maalumu ya Ukatili majumbani.
- ✓ Serikali inapaswa kupitia upya sheria zote zinazokinzana na kuzifanyia marekebisho ili kuhakikisha utekelezaji madhubuti wa vifungu vya kisheria ili kukomesha ukatili majumbani nchini Tanzania.
- ✓ Serikali inapaswa kuanzisha mahakama ya familia ambayo itasaidia kutoa maamuzi kwa haraka dhidi ya kesi za ukatili majumbani na kuhakikisha upatikanaji wa haki kwa waathirika.
- ✓ Serikali kwa kushirikiana na wadau, inapaswa kuimarisha mifumo ya taarifa za ukatili majumbani kwa kuanzisha na kuzijengea uwezo kamati za kuzuia ukatili wa wanawake na watoto.
- ✓ Serikali na wadau wa maendeleo wahakikishe wanatoa kipaumbele cha fedha kwa ajili ya programu zinazozuia na kukabiliana na ukatili dhidi ya wanawake na wasichana ndani ya familia na kwenye jamii.
- ✓ Serikali kwa kushirikiana na wadau kama vile Asasi za Kiraia, Sekta Binafsi na Taasisi za Kidini kuendelea kutoa elimu na uelewa juu ya kupunguza mila na desturi zinazochochea ukatili majumbani.

- ✓ Serikali inapaswa kufanya kazi bega kwa bega na wadau wengine ili kuboresha huduma za afya pamoja na kuanzisha zaidi makazi na nyumba salama kwa ajili ya wanawake na watoto ambao ni waathirika wa ukatili majumbani.

## Kuhusu Shirika la Wanawake Katika Sheria na Maendeleo Barani Afrika (WiLDAF)

Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Barani Afrika, ni mtandao wa mashirika ya watu binafsi katika Bara la Afrika ambao unafanya kazi za kupinga haki za wanawake, kujitolea kukuza na kuimarisha mikakati inayounganisha sheria na maendeleo ili kuongeza ushiriki wa ushawishi wa wanawake katika mikakati na pia kueneza chachu hiyo katika ngazi ya jamii, kitaifa na kimataifa.

WiLDAF ilisajiliwa nchini Tanzania mnamo mwaka 1997 chini ya Sheria ya Makampuni Sura ya 212 kama Shirika lisilo la kiserikali, lisilo la kisiasa na lisilojiendesha kwa faida.

WiLDAF Tanzania ina njozi ya kuona jamii ya Tanzania inayoheshimu haki za binadamu za wanawake. Misheni ni kujenga ni kujenga mtandao imara kwa ajili ya kukuza heshima kwa haki za binadamu za wanawake kupitia utetezi, usambazaji na uangalizi wa vyombo mbalimbali vya kitaifa na kimataifa pamoja na mpango wa dharura wa kuitikia ukatili wa kijinsia katika ngazi zote wakati huo huo ikihusisha sheria na maendeleo.

## Kuhusu Mradi wa Uchechemuzi kwa Kutumia Takwimu (DDA)

Mradi wa uchechemuzi kwa kutumia Takwimu (DDA) ni mradi unaofadhiliwa na Shirika la Kimataifa liitwalo Freedom House pamoja na PACT Tanzania.

Mradi huu ambao ni wa miaka mitano unakusudia pamoja na mambo mengine kutumia takwimu kama sehemu ya kushawishi mabadiliko ya Sera na Sheria ambazo zinalinda na kutetea haki za binadamu.

Mradi huu unafanya kazi kwa kupitia vikosi kazi (WGs) mbalimbali. WiLDAF inaratibu kikosi kazi namba mbili (WG2) ambacho kimejikita katika kusimamia haki za Wanawake,Watoto, Vijana na watu wenye ulemavu.

## SHUKRANI

Taarifa hii fupi ni mchango wa watu binafsi, mashirika na wanachama wa kikosi kazi namba 2 ambao kwa pamoja wameshiriki katika kuandaa taarifa hii.

Kwa niaba ya kikosi kazi namba 2 (WG2), WiLDAF inapenda kutambua juhudi iliyofanywa na muandishi Bwana Idd Rajabu Mziray kwa kujitolea kwake katika kuandaa rasimu ya awaliya taarifa hii fupi.

Vile vile tunatoa shukrani kwa Mkurugenzi wa WiLDAF Anna Kulaya kwa kuhariri taarifa hii fupi.

WiLDAF inapenda kuwashukuru wafuatao kwa kupitia na kuchangia katika kuboresha taarifa hii fupi; Bi Zakia Msangi, Bi Miriam Azaria, Asajile Mwakyusa, Simoni Songeraeli, Michael Lwakatare pamoja na Bi Anneth Mushi.

Mwisho, shukrani ziende kwa wanachama wa WG2 ambao wameshiriki kikamilifu katika kuandaa taarifa hii fupi kama ifuatavyo;

1. Women in Law and Development in Africa (WiLDAF),
2. Tanzania Child Right Forum (TCRF),
3. Tanzania Domestic Workers Coalition (TDWC),
4. Mwanza Children and Youth Network (MCYN),
5. Tanzania Early Childhood Development Network (TECDEN),
6. Zanzibar Female Lawyers Association (ZAFELA),
7. Tanzania Association for children Advancement (ZACA),
8. Women Legal Aid Centre (WLAC),
9. Women with Disability Network (SHIVYAWATA),
10. Youth Partnership countrywide (YPC),
11. Gender and Adolescence Initiative (GAI)

12. Vijana Pambana Pata Maendeleo Rukwa (VIPAMARU),

13. Jitambue Lembuka,

14. Health Integrated Multispectral Services (HIMS),

15. Women Development for Science and Technology Association (WODSTA).

## MAREJEO


1. Ufahamu wa wasichana na harakati za ufeminist (2014). Utafiti juu ya Mitazamo na Mitazamo ya Watu kuelekea Ukatili wa Ndani nchini Pakistan. Wasichana wanaofahamu, Vijana wa Feminists Movement Mama Cash.
2. Shirika la kimataifa la Amnest (AI). 25 Februari 2015. "Tanzania." Ripoti ya shirika na kimataifa la Amnest 2014/15: Hali ya haki za binadamu duniani. [Imepitiwa 6 Julai 2021]
3. Jumuiya ya Afya ya Jamii ya Canada "Afrika" (CACHA). NDA. 'Kuhusu Sisi.' [Imepitiwa 6 Julai 2021]
4. 'Pamoja Wanawake Centre Project- Zuia Ukatili kwa Uwezeshaji wanawake - Moshi Tanzania.' [Imepitiwa 7 Julai 2021]
5. Gazeti la "The Citizen" [Tanzania]. 25 Juni 2015. Leila Sheikh. "Tanzania inahitaji sheria ya Ukatili majumbani kwa haraka." [imepitiwa 25 June 2021]
6. Deutsche Welle (DW). 3 Decemba 2013. 'Tanzania Yapiga Hatua Dhidi ya Ukatili wa Kijinsia.' [Imepitiwa 2 Julai 2021]
7. Freedom House. 2015. "Tanzania." Uhuru Duniani 2015. [Imepitiwa 2 Julai 2015]
8. Human Development Trust (HDT). Juni 2011. Mapungufu katika Sera na Sheria zinazoendeleza ukatili wa kijinsia nchini Tanzania. [Imepitiwa 2 Julai 2015]N.d. "Who We Are." [Accessed 2 July 2021]
9. Kituo cha Kimataifa cha Utafiti juu ya Wanawake (ICRW). N.d. 'Sisi ni nani.' [Imepitiwa 29 Julai 2021]
10. Waandishi wa habari wa Haki za Binadamu (J.H.R.). 14 Januari 2014. Brielle Morgan. 'Kupambana na Ukatili wa Kijinsia Dar es Salaam- Siku 16 na Zaidi.' [Imepitiwa 2 Julai 2015]
11. Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC). N.d. 'Kuhusu Sisi.' [Imepitiwa 6 Julai 2015]
12. Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu Zanzibar (LHRC) na Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC). mwezi Machi 2014. Ripoti ya Haki za Binadamu Tanzania ya mwaka 2013. [Imepitiwa 6 Julai 2021]

13. McCleary-Sills, Jennifer, Sophie Namy, Joyce Nyoni, Darius Rweyemamu, Adrophina Salvatory, Ester Steven. March 2013. Kituo cha Kimataifa cha Utafiti juu ya Wanawake. Njia za Kutafuta Msaada na Vikwazo kwa Waathirika wa Ukatili wa Kijinsia nchini Tanzania. [Imepitiwa 9 Julai 2021]

14. Reuters. 25 Julai 2013. Kizito Make. “Ukatili wa Kijinsia Nchini Tanzania.” [imepitiwa 3 Julai 2021]

15. Southern African Legal Assistance Network (SALAN). N.d. ‘Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (Zanzibar).’ [Imepitiwa 7 Julai 2021]

16. Tanzania: Utafiti wa Idadi ya Watu na Afya, (TDHS) 2015/2016

17. TAWLA, Septemba 2014: Mapitio ya Sheria na Sera zinazohusiana na Ukatili wa Kijinsia Tanzania Bara

18. UNICEF Tanzania, CDC, na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi cha Muhimbili. 2011. Ukatili dhidi ya watoto nchini Tanzania: Matokeo ya Utafiti wa Kitaifa wa 2009. Dar es Salaam, Tanzania. *Takwimu za maambukizi zinaweza kutofautiana na ripoti kutokana na uchambuzi wa ziada unaozingatia watoto wa umri wa miaka 18-24

ISBN 978-9912-9860-0-8

**Imechapishwa na WiLDAF, 2021**
Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo barani Afrika
Eneo la Mikocheni A. Mtaa wa WiLDAF, Block F. Ploti Na. 635.
S.L.P 76215, Dar es salaam, Tanzania

**Simu:** +255222701995,
**Barua pepe:** wildaftanzania@gmail.com / info@wildaftanzania.or.tz
**Tovuti:** www.wildaftanzania.or